

Uchambuzi wa mambo ya kitamaduni yanayowakwamisha wanawake kushiriki katika shughuli za uchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu, Mwakitolyo, mkoa wa Shinyanga

Thubutu Africa Initiatives
Septemba 2025

Muhtasari

Ushiriki wa wanawake katika shughuli za uchimbaji mdogo wa dhahabu nchini Tanzania, hususani katika kijiji cha Mwakitolyo kilichopo wilayani Shinyanga, bado unakabiliwa na vikwazo vikubwa vinavyotokana na mila na desturi zilizojengeka kwa muda mrefu katika jamii. Vikwazo hivi vya kijamii na kitamaduni vinaonesha hitaji la kufanya utafiti wa kina ili kuelewa chanzo chake na athari zake, na kusaidia kuandaa mikakati maalum ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika sekta hiyo.

Utafiti huu ulifanyika katika kijiji cha Mwakitolyo na ulilenga kuchunguza vikwazo hivyo kupitia maswali yafuatayo ya utafiti:

1. Ni mila na desturi gani kuu zilizopo **katika** Mwakitolyo zinazozuia ushiriki wa wanawake katika shughuli za uchimbaji wa dhahabu?
2. Ni athari gani za kiuchumi na kijamii zinazosababishwa na kuzuia ushiriki wa wanawake katika shughuli za uchimbaji wa dhahabu Mwakitolyo?
3. Ni mikakati ipi au aina gani ya hatua zinaweza kusaidia kushughulikia vikwazo vinavyozuia ushiriki wa wanawake katika uchimbaji wa dhahabu Mwakitolyo?

Utafiti ulitumia mbinu za kidadisi (qualitative), ikiwa ni pamoja na mahojiano na wadau muhimu, mahojiano ya kina yaliyoelekezwa kwa sehemu, mijadala ya vikundi lengwa, na uchunguzi wa moja kwa moja. Jumla ya washiriki 50 walihusishwa katika utafiti huu, wakiwemo wanawake wachimbaji, wanawake walioko katika biashara zinazohusiana na uchimbaji, wachimbaji wanaume, pamoja na viongozi wa serikali za mitaa na wawakilishi wa asasi za kiraia.

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa vikwazo vikuu vinavyozuia ushiriki wa wanawake katika uchimbaji mdogo wa dhahabu Mwakitolyo vinatokana na imani potofu kuhusu hedhi na ujuzito, mitazamo ya kijinsia inayoweka mipaka ya majukumu ya wanawake, na tamaduni za Kisukuma zinazowapa wanawake nafasi ya kwanza kama walezi wa familia. Imani na matarajio haya yanawazuia wanawake kushiriki katika nafasi zenye kipato kikubwa au kazi ngumu za uchimbaji ambazo mara nyingi huhusishwa na wanaume. Zaidi ya hayo, changamoto za kiuchumi kama vile ukosefu wa zana za uchimbaji, mitaji, na mikopo vinachangia kuwafanya wanawake washindwe kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi kupitia madini.

Kutengwa kwa wanawake katika sekta ya madini kunachochea ukosefu wa usawa wa kiuchumi na kijinsia, kunazuia uwezo wao wa kiuchumi, na kuwaweka kwenye hatari zaidi ya umasikini. Vilevile, uwakilishi mdogo wa wanawake katika vyombo vya maamuzi unaendelea kutengwa kwao na kuzuia maendeleo jumuishi katika uchumi wa eneo hilo.

Licha ya changamoto hizo, utafiti umetambua mikakati yenye matumaini ya kusaidia ushiriki mkubwa wa wanawake katika shughuli za uchimbaji **mdongo** wa dhahabu. Mikakati hiyo ni pamoja na: (1) uanzishaji wa programu za uhamasishaji na utoaji wa elimu kwa jamii ili kupambana na mitazamo potofu na imani za kijadi, na (2) kutoa mafunzo ya kiufundi, ujasiriamali, na uendeshaji wa biashara kwa wanawake ili kuwawezesha kushiriki kwa tija na kujitegemea katika sekta ya uchimbaji.

Ili kuongeza ushiriki wa wanawake, utafiti unapendekeza juhudi za pamoja zinazolenga elimu na uhamasishaji, ujenzi wa uwezo, kuimarisha mitandao ya wanawake, pamoja na kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha na vifaa vya uchimbaji.

Kwa kumalizia, kushughulikia vikwazo vya kijamii, kiuchumi na kimfumo vinavyozuia ushiriki wa wanawake katika sekta ya madini ni muhimu siyo tu kwa ajili ya kuendeleza usawa wa kijinsia, bali pia kwa kuleta maendeleo endelevu katika sekta ya uchimbaji wa dhahabu Mwakitolyo na jamii kwa ujumla. Kujenga mazingira jumuishi ambapo wanawake wanaweza kushiriki kikamilifu katika nyanja zote za uchimbaji wa dhahabu kutaboresha hali ya kiuchumi ya wanawake na familia zao na kuchangia maendeleo jumuishi na yenye uthabiti katika ngazi ya jamii.